

WATOTO WACHANGA WENYE VIRUSI VYA UKIMWI

Ugonjwa wa ukimwi unaendelea kuenea , virusi vya ukimwi unaenea kwa watu wadogo sana sana na zaidi ya watu asilimia tisini na tano(95%) wana ugonjwa huu katika nchi zinazoendelea na kati ya hawa asilimia tisini na tano(95%) wanaaga dunia.

Wengi wa watoto wenyе virusi vya ukimwi wanapata virusi hivi kutoka kwa mama zao kwa kupitia kunyonyesha au wakati wa kuzaa , wanasayansi wana dhani ya kwamba virusi vya ukimwi hupitishiwa mtoto wakati damu ya mama yake huingia mwilini mwa mtoto.Njia zingine zinazoeneza virusi kutoka kwa mama hadi mtoto ni kama vile wakati mwingi unapita kati ya kusikia uchngu wa kuzaa na wakati wa kuzaa na damu ya mama inashikana na mtoto.Pia watoto wengine na pia watu wazima wanaweza kuambukizwa virusi hivi kwa njia ya kuongezewa damu yenye virusi au kwa kunajisiwa na mtu mwenye virusi vya ukimwi.

Utafiti unaonyesha yakwamba kunyonyesha watoto unahatari ya asilimia kumi hadi kumi na tano(10% -- 15%) ya kuambukiza virusi , kwa hivyo ni muhimu sana kuelezea wamama hatari na maana ya kunyonyesha watoto.Nchi ambazo zinaweza kusaidia wamama kutumia njia zingine ya kulisha wanawe zina himizwa kufanya hivyo.

Virusi vya ukimwi huenea kwa njia mbili kwa watoto; asilimia ishirini(20%) ya watoto wenyе virusi wanakuwa wagonjwa sana katika mwaka wao wa kwanza wa maisha na kufa wakiwa na miaka nne , na asilimia themanini (80%) huenea polepole. Watoto wengi huongeza kilo polepole ,akili na mwili pia hukua polepole kama vile kutambaa,kutembea ,kuongea,na pia masomoni. Kama watu wazima watoto hao hushikwa na magonjwa tofauti kila wakati kama vile candida . lakini ugonjwa ambao huleta kifo ni pneumonia .Watoto wenyе virusi hushikwa na magonjwa mengi ya

kitoto na mingi huwa hatari kama vile joto , kuharisha na pneumonia.

Ni vigumu kupima virusi kwa watoto wachanga kwani wengi wao huonekana wenye afya.Na pia watoto wana protini ya antibody ambayo huwapatia kinga kwa miezi kumi na nane na hii inafanya vigumu kupima virusi.

Watoto wenye wamezaliwa na wamama wenye virusi wanafaiwa kupimwa virusi wakati wa kuzaliwa ,wakiwa na wiki nne hadi saba na wakiwa na wiki nane hadi kumi na sita. Matokeo yakionyesha virusi vya ukimwi basi wanafaiwa kupimwa mara ya pili ili kuhakikisha.

Kipimo moja ambayo inaitwa polymerase chain reaction (PCR) inatumwa kupima virusi na huonyesha kiwango cha virusi mwilini na inaaminiwa kuwa na uhakika.

Njia nyingine ya kupima ni kwa kugandisha damu ya mtoto ili ionyeshe virusi vya ukimwi, kwa kutumia njia hizi karibu asilimia tisini(90%) ya watoto wanapimwa wakiwa na miaka miwili na asilimia tisina na tano(95%) wakiwa na miezi mitatu .

Kwa wakati wote uwezekanapo virusi vya ukimwi vinapaswa kutambuliwa kabla au wakati wa mimba kwa ni hii inapea mama muda wa kutosha kumkinga mtoto wake kutokana na virusi vya ukimwi. Pia madawa mengine yakiunganishwa husaidia kwa kukingga mtoto asiambukizwe virusi vya ukimwi kama vile AZT ambayo hupewa mama akiwa na mimba ya miezi mitatu ama miezi sita na kuendelea mpaka azae lakini madawa haya ni ghali na watu wengi hawawezi pata .Utafiti unaonyesha madawa ya muda mfupi kama vile nevirapine huteremsha hatari ya mtoto kuambukizwa virusi katika wiki ya kumi na nane kwa asilimia hamsini (50%).Mapato haya yanatumwa na nchi zinazoendelea kwani ni rahisi kushinda AZT .

Pia kupasuliwa wakati wa kuzaa huteremsha hatari ya kuambukiza

virusi ikitumiwa pamoja na AZT.

Madawa ambayo hutumiwa kwa watoto wenyewe virusi vya ukimwi ni :

1-Nucleoside Reverse Transcriptase Inhibitors kama vile Lamivudine na Zidovudine.

2-Nonnucleoside Reverse Transcriptase Inhibitors kama vile delaviridine na nevirapine.

3-Protease Inhibitors kama vile amprenavir natipranavir.

4-Fusion Inhibitors kama vile enfuvirtide.